## AckySHINE.com

# Mama mwenye virusi vya UKIMWI na UKIMWI, anaweza kuzaa mtoto?

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Na anaweza kumwambukiza mtoto aliye tumboni au wakati wa kumnyonyesha? Ndiyo, mama mwenye virusi vya UKIMWI na UKIMWI anaweza kubeba mimba kama mwanamke mwingine yeyote. Ila ni muhimu kukumbuka kwamba kuna uwezekano wa mtoto kuambukizwa na Virusi vya UKIMWI.

Lakini siyo watoto wote waliozaliwa na mama mwenye maambukizi watabeba virusi. Kuwa moto ataambukizwa au hataambukizwa i itategemea na i idadi ya virusi ambavyo viko kwenye damu ya mama na sababu nyingine. Tafiti zimeonyesha kwamba watoto wawili kati ya watoto watatu waliozaliwa na akina mama wenye maambukizi ya Virusi huambukizwa na hivyo virusi. Pamoja na hayo, mama mwenye virusi vya UKIMWI anaweza kumwambukiza mtoto wake wakati wa kumnyoshesha kwa sababu ya kuwepo virusi kwenye maziwa ya mama. Akina mama walio na maambukizi ya UKIMWI na UKIMWI wanashauriwa kuacha kuzaa na kutumia njia za uzazi wa mpango